

## TANGAZO KWA UMMA

### MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MANYONI (“MANYONI WSSA”) KWA MWAKA 2017/18 – 2019/20

#### Maombi ya mabadiliko ya Bei Na. TR-W-17-10

Mnamo tarehe 20 Juni 2017, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea ombi kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Manyoni (Manyoni WSSA) la kutaka kuongeza bei ya huduma zake za majisafi kwa mwaka 2017/18 hadi 2019/20. Jedwali namba 1 hadi 6 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

#### Jedwali 1: Bei za Maji sasa na zinazopendekezwa (shilingi kwa mita moja ya ujazo)

Aina za wateja	Matu mizi (m <sup>3</sup> )	Bei za sasa	Bei Zilizopendekezwa			
		2016/17	% Ongezeko	2017/18	% Ongezeko	2018/19-2019/20
Majumbani	1	540	270%	2000	0%	2000
Biashara	1	795	277%	3,000	0%	3,000
Taasisi	1	550	445%	3,000	0%	3,000
Viwandani	1	0	NA	3,500	0%	3,500
Magati	1	1000	150%	2,500	0%	2,500

#### Jedwali 2: Gharama ya Huduma ya Sasa na Iliyopendekezwa (shilingi/mwezi)

Aina za wateja	Bei za sasa	Gharama Zilizopendekezwa			
	2016/17	% Ongezeko	2017/18	% Ongezeko	2018/19-2019/20
Majumbani	540	270%	2,000	0%	2,000
Biashara	795	277%	3,000	0%	3,000
Taasisi	550	445%	3,000	0%	3,000
Viwandani	0	NA	3,500	0%	3,500
Magati	1,000	150%	2,500	0%	2,500
Manywesheo ya mifugo	0	NA	2,500	0%	2,500

**Jedwali 3: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Maunganisho Mapya (Shilingi kwa Unganisho Jipya)**

Aina za wateja	Bei za sasa	Tozo Zilizopendekezwa	
	2016/17	% Ongezeko	2017/2018-2019/20
Majumbani	46,500	51%	70,000
Biashara	47,500	68%	80,000
Taasisi	47,000	70%	80,000
Viwandani	0	NA	90,000

**Jedwali 4: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kusitishwa (Shilingi kwa marejesho)**

Aina za Wateja	Bei za sasa	Tozo Zilizopendekezwa			
	2016/17	% Ongezeko	2017/2018	% Ongezeko	2018/2019-2019/20
Majumbani	10,500	43%	15,000	0%	15,000
Biashara	11,000	82%	20,000	0%	20,000
Taasisi	11,000	82%	20,000	0%	20,000
Viwandani	0	NA	25,000	0%	25,000

**Jedwali 5: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Mita ya Maji kwa Mteja (Shilingi kwa mwezi)**

Aina za wateja	Bei za sasa	Tozo Zilizopendekezwa			
	2016/17	% Ongezeko	2017/18	% Ongezeko	2018/2019-2019/20
Majumbani	500	100%	1,000	0%	1,000
Biashara	500	100%	1,000	0%	1,000
Taasisi	500	100%	1,000	50%	1,500
Viwanda	0	NA	1,500	0%	1,500

**Jedwali 6: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Fomu ya Maombi ya Kujiunga na Huduma ya Maji kwa Mteja Mpya (shilingi/fomu)**

Aina za wateja	Bei za sasa	Tozo Zilizopendekezwa	
	2016/17	% Ongezeko	2017/2018-2019/20
Majumbani	5000	0%	5000
Biashara	5000	0%	5000
Taasisi	5000	0%	5000
Viwandani	0		5000

Kutokana na wasilisho la Manyoni WSSA, bei zinazopendekezwa zitaiwezesha Manyoni WSSA kuongeza mapato ili kumudu gharama za uendeshaji na matengenezo, kupanua mtandao wa usambazaji majisafi kwenye makazi mapya na kuweza kupata fedha ya kulipia uchakavu wa miundombinu ya majisafi.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Ijumaa, tarehe 20 Oktoba, 2017 katika Ukumbi wa Maktaba, Manyoni Mjini** kuanzia saa **4:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu ndani ya kipindi kabla ya tarehe **27 Oktoba, 2017**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi ya EWURA, **GHOROFA YA NNE, WING A, LAPF HOUSE, MAKOLE ROAD, S.L.P 2857 DODOMA**; au ofisi za **Manyoni WSSA** zilizoko mjini Manyoni.

**Imetolewa na:**  
**Kaimu Mkurugenzi Mkuu**  
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)**  
**20 Septemba 2017**